

Jinsi ya kutuma ombi kwa usaidizi wa Sehemu ya 4 iwapo wewe ni mjamzito



Oktoba 2010

Swahili

Sehemu ya 4 ni usaidizi wa muda mdogo unaotolewa na Ofisi ya Nyumbani iwapo utafutaji kimbilio wako umekataliwa, na rufaa zako zimekuwa bila mafanikio. Iwapo huwezi kutoa Uingereza mara moja na vinginevyo kuwa bila makao au bila pesa za kununua chakula (yaani uko fukara), unaweza kustahili kupata usaidizi wa Sehemu ya 4 ukiwa mjamzito.

Hata hivyo, ili kutuma ombi la usaidizi wa Sehemu ya 4 kwa sababu ya ujauzito wako, Ofisi ya Nyumbani huhitaji utoe nyaraka hizi **zote**. Unapokusanya maelezo yanayoelezwa hapa nchini rudi ofisini mwetu katika Halmashauri ya Wakimbizi ya Uskoti na tutapanga miadi ya Sehemu ya 4 kwa ajili yako.

Nyaraka unazohitaji ni pamoja na:

1. Hati ya A MATB1 kutoka kwa daktari wako (GP) **au** mkunga inayoonyesha kuwa una angalau wiki 32 za ujauzito. Iwapo hujamwona mkunga bado, tunaweza kupanga miadi kwa ajili yako;
2. Orodha iliyoandikwa kwa anwani ambazo umeishi tangu ulipofika Uingereza. Orodha hii lazima iwe katika mpangilio wa wendo kuanzia anwani za karibuni sana hadi kwa anwani za kwanza kabisa ulizoishi ulipowasili Uingereza. Weka nambari za watu ulioishi nao na ni kwa nini hawawezi kukusaidia tena. Hii ni muhimu sana kwa mkwaka wa mwisho kabla la ombi lako. Kama unweza pia kutoa barua zilizotumwa kwako katika anwani hizi, itasaidia ombi lako la Sehemu ya 4;

3. Orodha iliyoandikwa ya maeneo yote uliyofanya kazi tangu kuwasili kwako katika Uingereza, pamoja na karatasi za mishahara na fomu za P45, zilizotolewa ulipomaliza kazi, nab ado unazo. Iwapi umefanya kazi kinyume na sheria za Uingereza, hakukatukwa na athari mbaya kuhusu ombi lako la Sehemu ya 4 kama umeacha kufanya kazi sasa;
4. Tondoti za akaunti zozote za benki ulizokuwa nazo Uingereza, pamoja na taarifa za benki za miezi sita iliyopita; **na**
5. Iwapo uko katika uhusiano na babake mtoto wako, utapaswa kutoa anwani, tondoti za kazi na taarifa za benki kutoka kwake pamoja na taarifa iliyoandikwa ikieleza sababu yake kutoweza kukusaidia wewe na mtoto.

Muhimu: Barua unazotoa lazima ziwe katika Kiingereza. Hata hivyo, iwapo mtu anayetoa barua hizo hawezi kuandika Kiingereza, tungependekeza kuwa uzilete kwenye miadi yako nasi ili tuweze kukusaidia katika kuandika barua yako.

Orodha za anwani na mahali pa kazi zilizosemwa kwenye barua zinaweza kuandikwa katika lugha yako iwapo huwezi kuziandika kwa Kiingereza.